

02.04.2026

TANGAZO LA ZABUNI YA UTOAJI HUDUMA YA KISHERIA KWA KCU (1990) LTD
MSIMU 2026/2027

Zabuni na: KCU/CS/2026/2027/01

1. KCU (1990) Ltd inahitaji huduma ya Kisheria kwa mambo mbalimbali ya kiofisi. Mambo hayo ni ya ushauri wa kisheria kama, kuandaa madai na kujibu madai yanayoletwa dhidi yake, kuiwakilisha KCU(1990) Ltd katika mahakama na mabaraza ya Ardhi na nyumba ya Wilaya.
2. Kutokana na uhitaji wa huduma ya kisheria na kwa vile KCU (1990) Ltd ni taasisi ya wananchi yenye haki ya kushitaki na kushitakiwa, hivyo yanakaribishwa maombi ya zabuni kwa ajili ya kutoa huduma ya kisheria msimu 2026/2027.
3. Mwombaji awe na ofisi inayotoa huduma ya uwakili Bukoba Manispaa.
4. Mwombaji aambatishe nakala ya wasifu wa kampuni.
5. Mwombaji aambatishe nakala za kusajiliwa na mamlaka zinazotambulika.
6. Mwombaji ambatisha nakala ya mwanachama wa Tanganyika Law society
7. Mwombaji ataje gharama zote za kutoa huduma kisheria kuanzia na 'Retainership fee' na gharama nyingine.
8. Mwombaji aambatishe nakala ya usajili wa kampuni (BRELA), TIN, V AT pamoja na VRN.
9. Mwombaji aambatishe nakala zinaonesha vielelezo vya kazi alizowahi kufanya.
10. Ombi la zabuni liwe na jina, anwani halisi ya mwombaji na mahali Ofisi ilipo.
(Physical address)
11. Maombi yaambatane na ada ya TShs. 200,000/= ambazo hazitarejeshwa kwa mwombaji. Fedha hizo zilipwe kupitia A/C Namba **01J1055955002 General A/C**
12. Tathmini itafanywa kwa kuzingatia vigezo 3-11 vilivyo tajwa hapo juu.
13. Bahasha ya maombi ifungwe vizuri katika lakiri na kuandikwa juu yake:- **"MAOMBI YA ZABUNI YA UTOAJI HUDUMA YA KISHERIA MSIMU 2026/2027"** kwa anwani tajwa hapa chini,

MENEJA MKUU,
KCU (1990) LTD,
P.O BOX 5,
BUKOBA.

15. Bahasha hiyo iletwe kwa mkono katika Ofisi ya Manunuzi KCU kabla au mnamo tarehe 20.04.2026 saa 4.00 asubuhi siku ya Jumatatu na ufunguzi wa maombi yote utafanyika muda huo, waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa katika sherehe ya ufunguzi mara tu baada ya saa ya mwisho yakupokea zabuni.
14. Maombi yatakayochelewa, maombi yasiyokamilika, maombi yaliyowasilishwa kwa njia ya kieletroniki na maombi yasiyokuwepo siku ya ufunguzi hayatahusishwa na uchambuzi wa kumpata mzabuni.

